# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

**Anwani ya Simu:"UCHUNGUZI"**
**Simu Nambari: (027) 2645186**
**Nukushi: (027) 2647885**
**Barua Pepe:** rbctangal@pccb.go.tz
**Tovuti:** www.pccb.go.tz

**Barabara ya Hospitali ya bombo,**
**S.L.P 1953,**
**21105 TANGA,**
**TANZANIA.**

## TAARIFA KWA UMMA

**APRILI, 2022**

**Ndugu wanahabari,**

Ninawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ninawakaribisheni tena katika ofisi ya TAKUKURU (M) Tanga.

Kama ulivyo utaratibu wetu, tumemaliza robo ya tatu ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 hivyo tumeitana kwa lengo la kuuhabarisha umma kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Tanga kwa kipindi cha Januari – Machi 2022.

**Ndugu wanahabari,**

**UCHUNGUZI:**

Katika jukumu la Kuchunguza tuhuma au makosa ya Rushwa pamoja na njama za kutendeka kwa makosa hayo, TAKUKURU Mkoa wa Tanga imepokea Jumla ya Taarifa **141** na kati ya taarifa hizo, **82** ni za vitendo vya rushwa na taarifa **59** si taarifa za vitendo vya rushwa. Taarifa **82** zilizohusu Rushwa zilifunguliwa majalada ya uchunguzi ambapo taarifa **60** zinaendelea kuchunguzwa na taarifa **22** zimefungwa kutokana na kukosekana kwa ushahidi wa kuthibitisha tuhuma.

Kati ya taarifa **59** ambazo hazikuhusu vitendo vya rushwa, taarifa **56** watoa taarifa walielimishwa na kushauriwa namna mbadala za kutatua kero zao na taarifa **03** zimehamishiwa idara zingine kwa hatua zaidi.

Mchanganuo wa taarifa hizo **141** za malalamiko kisekta ni kama ifuatavyo: Serikali za mitaa **26**, Makampuni binafsi ya ulinzi 02, Mahakama **03**, Mashirika Binafsi **13**, Mashirika ya Umma **09** Mabaraza ya Ardhi **03**, Elimu **16**, Afya **11**, TAMISEMI (Utawala **09**, Manunuzi 5 Elimu 5, VEO 6, UJENZI 4, ARDHI 14 Majeshi ya Ulinzi na Usalama **05**,

taasisi za fedha 04**,** TASAF **03**, Sekta ya Maji **01**, na Idara ya Uvuvi **01** na Maliasili **01**.

Katika kipindi husika, TAKUKURU Mkoa wa Tanga imefungua mashauri **11** na kufanya jumla ya mashauri yanayoendelea mahakamani mpaka sasa kuwa **32**. Katika kipindi cha Januari – Machi 2022, Mashauri matatu **(03)** kati ya **35** yaliyokuwa yakiendelea mahakamani yalitolewa maamuzi ambapo mashauri mawili (**2**) watuhumiwa walikutwa na hatia na kutakiwa kulipa faini au kutumikia kifungo na shauri moja **(1)** watuhumiwa waliachiwa huru kwa kuwa hawakuwa na kesi ya kujibu.

**Ndugu wanahabari,**

**UZUIAJI RUSHWA:**

Katika utekelezaji wa jukumu hili, TAKUKURU Mkoa wa Tanga kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Machi 2022 tumefanya kazi za ufuatiliaji wa **miradi ya maendeleo 26** yenye thamani ya jumla ya **shs. 9,960,678,186.40/=** kwenye Sekta za Elimu, Afya na Barabara. Katika Ufuatiliaji huo, wilaya zote zilifuatilia ujenzi wa barabara zilizopo chini ya TARURA ambazo zilipata fedha kutoka Serikali kuu kwenda kwa kila Jimbo. Katika ufuatiliaji huu wa miradi kuna miradi miwili yenye thamani ya jumla ya sh **1,250,000,000/=** ilibainika na kasoro na uchunguzi umeanzishwa. Katika Mradi wa ujenzi wa Hospitali wilayani Handeni, tofali zilizochukuliwa kwa ajili ya ujenzi zilikuwa za gharama kubwa wakati kulikuwa na tofali aina hiyo ambazo bei ilikuwa chini. Pia katika ujenzi wa shule wilayani Muheza, wakati wa kupaua bati zilizotumika ni tofauti na zilizokuwa zimeainishwa kwenye BOQ.

**Ndugu wanahabari,**

TAKUKURU Mkoa wa Tanga pia tumefanya uchambuzi wa mifumo ili kupata tija ya mifumo imara isiyokwamisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Jumla ya chambuzi **11** za mifumo zimefanyika, katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa Mfumo wa utendaji kazi wa Wakala wa ufundi na umeme Tanzania (TEMESA) pamoja na uchambuzi wa mfumo wa usimamizi wa mapato yanayotokana na ushuru wa madini ya Ujenzi.

Kazi hii ya uchambuzi wa matumizi ya tozo zitokanazo na madini ya ujenzi imefanywa na Wilaya zote za Mkoa wa Tanga kwa sababu hii ni kazi ya kitaifa. Katika uchambuzi huo yafuatayo yalibainika:

- Machimbo mengi ya mchanga yana leseni zilizotolewa kutoka ofisi ya Madini, lakini hayana vibali kutoka ofisi ya Halmashauri husika

- Makusanyo yanayokusanywa kupitia Serikali za Vijiji na mitaa yanakusanywa kwa kutumia Vitabu vya mkono badala ya mashine za EFD
- Baadhi ya wachimbaji hawaweki mipaka kuzunguka eneo la uchimbaji na hivyo kupelekea uchimbaji kufanyika hadi nje ya eneo husika.
- Kutokuwepo kwa kumbukumbu zinazoonesha idadi ya magari yanayobeba madini ya ujenzi na pia
- Baadhi ya wachimbaji kutozingatia taratibu za utunzaji wa mazingira ikiwemo kufukia mashimo na kupanda miti baada ya uchimbaji.

Kutokana na matokeo hayo, TAKUKURU Mkoa wa Tanga ilizishauri Mamlaka husika kuhakikisha kuwa zinasimamia sheria, kanuni na taratibu ili kuhakikisha makusanyo ya mapato kupitia uchimbaji huo yanapatikana na utunzaji wa mazingira unafanyika ikiwa ni pamoja na Halmashauri kuona umuhimu wa kusambaza mashine za EFD katika Serikali za vijiji na mitaa ili makusanyo yaweze kukusanywa kwa njia za mashine za kielektroniki.

Aidha, katika kipindi husika zimefanyika warsha **06** na wadau - kujadili matokeo ya chambuzi zilizofanyika na kuwekeana mikakati ili kuondoa mapungufu yaliyobainika pamoja na mianya ya rushwa.

**Ndugu waandishi wa Habari,**

**UELIMISHAJI UMMA:**

Katika kipindi husika, TAKUKURU Mkoa wa Tanga imefanya jumla ya semina **35;** Mikutano ya hadhara **64; V**ipindi vya redio **15** na maonesho **07**. Lakini pia tumeandika Habari na Makala **13;** Tumetoa taarifa **1** kwa umma na pia tumeimarisha jumla ya klabu **177** katika shule na vyuo mbalimbali hapa mkoani Tanga.

Kupitia ushirikiano wa TAKUSKA, tumeweza kuwahamasisha na kuwapa elimu Viongozi na Vijana ambao ni wanachama wa Skauti katika shule za sekondari na msingi na hivyo kupelekea uimarishaji wa Klabu za Wapinga Rushwa.

**Ndugu wanahabari,**

**MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI**

TAKUKURU Mkoa wa Tanga tumeshiriki katika MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI, yaliyofanyika nchi nzima tarehe 08.03.2022. Katika matukio tangulizi ya Siku ya Wanawake Duniani, mnano tarehe 7/03/2022 TAKUKURU wilaya ya Muheza, ilifanya mdahalo na mjadala wa wazi katika ukumbi wa Tate plus, uliohusu 'Nafasi ya mwanamke katika mapambano dhidi ya rushwa ya ngono.' Mdahalo huo ulihudhuriwa na viongozi mbalimbali wakiwemo madiwani wanawake, walimu wakuu, walimu wa kawaida na wanafunzi wa shule za sekondari na msingi wakiongozwa na Katibu Tawala Wilaya ya Muheza - Bi Desderia Haule ambaye alikuwa mgeni rasmi.

**MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA NCHINI**

**Ndugu wanahabari,**

Kwa Upande wa Maadhimisho ya Wiki na Siku ya Sheria, yaliyofanyika kuanzia tarehe 23.01.2022 na kuhitimishwa tarehe 02.02.2022, TAKUKURU Mkoa wa Tanga imeshiriki katika Uelimishaji Umma kwa njia ya maonesho, semina, Vipindi vya Redio na Televisheni pamoja na Mikutano ya Hadhara.

**SUCCESS STORY (JAMBO LA MAFANIKIO)**

**Ndugu wanahabari,**

Mnamo tarehe 25.02.2022, ikiwa ni siku ndani ya wiki ya maandalizi kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, TAKUKURU mkoa wa Tanga na wilaya zake ilifanya kongamano katika Chuo cha Afya na Tiba na Sayansi Shirikishi Tanga (BOMBO) lililohusu nafasi ya mwanamke katika mapambano dhidi ya rushwa. Kongamano lilihudhuriwa na makundi mbalimbali ya wanawake na wa rika tofauti. Wageni waalikwa katika kongamamno hilo walikuwa ni pamoja na Mkuu wa Chuo cha Uuguzi Bombo Dkt. Lucheri Kweka, Kamishna wa Skauti Jiji la Tanga Bw. Mpiano Sitta Juma, ambapo Mgeni Rasmi alikuwa ni Afisa Elimu (M) Tanga - Bi Newaho Mkisi ambaye alimwakilisha Katibu Tawala Mkoa wa Tanga.

Mafanikio tuliyoyapata katika kongamano hili ni kuwakutanisha, wanawake wa rika tofauti na taaluma mbalimbali waliojadili nafasi yao katika mapambano dhidi ya Rushwa hususani Rushwa ya Ngono na kisha kupanga mikakati na mbinu za kuweza kuimarisha mapambano dhidi ya

Rushwa katika harakati mbalimbali zinazomhusu mwanamke. Washiriki hao walitumia fursa hiyo kuwaasa wanachuo na wanafunzi wasichana kujiandaa kuwa walezi bora wa kizazi kitakachosaidia kudhibiti vitendo vya Rushwa na hivyo kuwa vinara katika Kuzuia Rushwa ya ngono.

**Ndugu wanahabari,**

**MIKAKATI YA APRILI – JUNI 2022.**

Mkakati wetu kwa kipindi cha Aprili hadi Juni 2022 ni kufanya kazi kwa kujielekeza katika KUZUIA RUSHWA. Hii ni pamoja na Ufuatiliaji wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Udhibiti wa mianya ya Rushwa pamoja na uelimishaji wa jamii.

**HITIMISHO:**

Nawakumbusha tena wakazi wa Mkoa wa Tanga na wadau wote kwa ujumla kupitia ninyi waandishi wa habari, kuendelea kutupa ushirikiano wakati wote katika mapambano dhidi ya Rushwa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa jukumu tulilopewa wote kwa mujibu wa Kifungu cha 39 (1) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11/2007.

Kifungu hiki kinatamka wazi kwamba kila mtu ambaye ana taarifa juu ya mtu kutenda kosa au kusudio la mtu kutenda kosa chini ya sheria hii, awe anafahamu kabla au baada ya kosa kutendwa, anatakiwa kutoa taarifa TAKUKURU. Hivyo basi Kwa yeyote mwenye taarifa inayohusu vitendo vya rushwa, asisite kufika katika ofisi yetu ya mkoa iliyopo BOMBO AREA karibu na HARBOURS CLUB na kwa wale waishio wilayani wasisite kufika katika ofisi za TAKUKURU zilizopo katika Wilaya husika.

Pia mnaweza kupiga simu ya dharura namba 113 au ukatuma ujumbe mfupi wa maandishi kwa kupiga *113# na kufuata maelekezo. Huduma hii ni BURE.

**Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.**

Imetolewa na:
**Zainabu Bakari**
MKUU WA TAKUKURU (M)
TANGA
**Simu 0738150225**